

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA



Barabara ya
Kilimatinde Cheyo,
S.L.P. 1020,
45112

TABORA,

Barua Pepe: rbctabora@pccb.go.tz.

TANZANIA.

www.pccb.go.tz

TAARIFA KWA UMMA

TABORA, 03 FEBRUARI, 2021

AGIZO LA RAIS LA KUWAREJESHEA WANANCHI FEDHA WALIZODHULIMIWA KWENYE MAJI LAKAMILIKA

Habari ya mchana Ndugu wanahabari,

Mtakumbuka tarehe 29 Januari 2021 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt John Pombe Joseph Magufuli akiwa njiani maeneo ya Busondo kuelekea Tabora aliagiza TAKUKURU mkoa wa Tabora kuchunguza ndani ya siku saba na kurejesha fedha zilizochangwa na wananchi kwa ajili ya mradi wa maji.

Napenda kuujulisha umma kuwa TAKUKURU mkoa wa Tabora ndani ya siku tatu tumekamilisha utekelezaji wa agizo la Mhe. Rais na kwamba leo Februari 3, 2021 tunarejesha fedha za wananchi walizokuwa wamechanga kama mchango wa jamii katika mradi wa maji fedha hizo hazikutumika kama ilivyokusudiwa.

Operesheni iliyofanywa na maafisa wa TAKUKURU mkoa wa Tabora imebaini kwamba mwaka 2010 na mwanzoni mwa mwaka 2011 wananchi

wa vijiji vya Upungu na Isuna vilivyoko Kata ya Puge Wilaya ya Nzega mkoani hapa, walichanga fedha kiasi cha Shs.6, 774,850/=.

Mradi huo haukutekelezwa na hata hivyo, imebainika kwamba, licha ya mradi kutotekelezwa wananchi waliokuwa wamechanga hawakurejeshewa fedha walizochanga.

TAKUKURU Mkoa wa Tabora tumekamilisha uchunguzi wa awali uliolenga kwanza kurejesha fedha za wananchi wanyonge zilizochangwa na wananchi wa vijiji vya Upungu na Isuna, hivyo leo tunakabidhi fedha zote zilizochangwa na wananchi hao ambazo ni kiasi cha shs 6,774,850/=.

TAKUKURU mkoa wa Tabora tutaendelea kufanya uchunguzi zaidi dhidi ya waliohusika na kadhia hii na wote watakaobainika kukiuka taratibu na sheria hatua stahiki zitachukuliwa dhidi yao.

Aidha, katika hatua nyingine, katika kuhakikisha kuwa wananchi wanaodhulumiwa na kuonewa wanapata haki zao, leo TAKUKURU mkoa wa Tabora inamrejeshea Mzee Amani Gomba (80) fedha zake kiasi cha shs 800,000/= alizokuwa amedhulumiwa na Afisa Ushirika wa Wilaya ya Urambo mkoani Tabora.

Uchunguzi wa TAKUKURU mkoa wa Tabora ulibaini kwamba Mzee Gomba alimpa Bw. Jumanne Kitundu - Afisa Ushirika wa Wilaya ya Urambo kiasi hicho cha fedha ili aweze kuwasaida yeye na wenzake kuandikisha ushirika wao wa ufugaji nyuki. Matokeo yake, Jumanne Kitundu hakuandikisha umoja huo na wala hakurudisha fedha alizokabidhiwa tangu mwaka 2016 licha ya kukumbushwa kuzirejesha mara kwa mara.

Vilevile, TAKUKURU Mkoa wa Tabora leo inamrejeshea Bw. Maundu Nyangasi shs.1,000,000/= fedha alizokuwa akim dai Mwl. Ramadhani Mtiba tangu mwaka 2019 bila mafanikio baada ya kumuzia duka la dawa.

Katika hatua nyingine, leo tunakabidhi kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Uyui Shs. 11,605,100/= fedha zilizookolewa na TAKUKURU Wilaya ya Uyui. Fedha hizi zilikusanywa kwa njia ya POS na baadhi ya watumishi na mawakala waliokabidhiwa jukumu la kukusanya mapato lakini hazikuwasilishwa serikalini.

Ninawashukuru sana wananchi wa Mkoa wa Tabora kwa ushirikiano mnaoutoa kwa TAKUKURU. Niwatake watumishi wote katika Mkoa wa Tabora kufanya kazi kulingana na taratibu na sheria, kila aliyepewa jukumu atekeleza kwa uadilifu.

Niwaombe wale wote wanaokosa nafasi ya kufika katika ofisi zetu mjitokeze kwenye maeneo tunayopita kusikiliza kero zenu kwani TAKUKURU tumeanzisha **huduma ya ofisi inayotembea**. Tunakuja kwenye makazi yenu hivyo tafadhali mjitokeze kwa wingi na kuwasilisha kero zinazowakabili.

Vile vile mnaweza kuwasiliana nasi kupitia simu ya dharura **namba 113** huduma hii ni bure kwa mitandao yote ya simu au mnaweza kuwasiliana nasi kupitia **TAKUKURU APP**.

Asante
Imeandaliwa na



Musa Chaulo

MKUU WA TAKUKURU MKOA